

GHOROFYA YA SITA, HARBOUR VIEW TOWERS, MTA A WA SAMORA, S. L. P. 72175 DAR ES SALAAM,  
TANZANIA

SIMU: (+255-22) 2123850; 2123853; 2123854; 2123856; FAX: (+255-22) 2123180  
Barua pepe: [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz) Wavuti: <http://www.ewura.go.tz>

## **TAARIFA KWA UMMA**

### **WITO WA KUKUSANYA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA KUPITISHIWA KANUNI YA KUKOKOTOA BEI ZA UMEME YALIYOWASILISHWA NA KAMPUNI ZA *ARTUMAS GROUP & PARTNERS (POWER) LIMITED NA UMOJA LIGHT COMPANY LIMITED***

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi kutoka kampuni za **Artumas Group and Partners (Power) Limited** na **Umoja Light Company Limited** (“Waombaji”), zitakazotumika katika Mikoa ya Mtwara na Lindi, kama ifuatavyo:

1. Kanuni ya Kukokotoa Bei ya Umeme wa Jumla; na
2. Kanuni ya Kukokotoa Bei ya Umeme wa Rejareja.

Kwa mujibu wa Kifungu Na.19(2)(b) cha Sheria ya EWURA (Sura ya 414), EWURA imeanza mchakato wa kukusanya maoni ili kubaini uhalali wa maombi yaliyowasilishwa.

Kanuni hizo za kukokotoa bei za umeme zitakapoidhinishwa na EWURA zitatumika kwa muda wa miaka 20 ya uendeshaji kuanzia siku ya makabidhiano ya miundombinu ya umeme kutoka TANESCO kwenda kwa Kampuni ya Umoja Light mwaka 2011. Bei zitakazotokana na kanuni hizo zitatumika katika Wilaya za Mtwara, Lindi, Masasi, Nachingwea, Newala, Tandahimba na Ruangwa.

Wananchi wote mnakaribishwa kuwasilisha maoni yenu kwa maandishi na/au kushiriki katika mikutano itakayofanyika siku ya **Jumanne, tarehe 29 Desemba 2009 mjini Mtwara (Ukumbi wa VETA); Jumatano, tarehe 30 Desemba 2009 mjini Lindi (Hoteli ya Kagwa); na Jumanne, tarehe 5 Januari 2010 jijini Dar es Salaam (Ukumbi wa Karimjee).**

Wadau watakaopenda kuchangia hoja kuhusiana na maombi tajwa wanatakiwa kujiandikisha EWURA kabla ya saa 11:00 jioni siku ya Jumatano tarehe **23 Desemba 2009**. Wadau wote watakaojitokeza kutoa hoja watapata muda wa kuwasilisha maoni yao katika mikutano hiyo. Wadau wengine ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na EWURA (Consumer Consultative Council - CCC), Baraza la Ushauri la Serikali (Government Consultative Council – GCC) na wananchi kwa ujumla watatoa maoni yao katika mikutano itakayofanyika kuanzia saa nne (4) kamili asubuhi katika kumbi mtakazofahamishwa baadaye.

EWURA inakaribisha maoni kwa maandishi kuhusiana na maombi husika ambayo yanatakiwa yawasilishwe kabla ya saa **11:00 jioni**, Ijumaa tarehe **15 Januari 2010**.

Taarifa za ziada kuhusiana na maombi haya zinapatikana bure katika wavuti wa EWURA ([www.ewura.go.tz](http://www.ewura.go.tz)), isipokuwa nyaraka za siri zilizowasilishwa na Waombaji zitasitiriwa kwa mujibu wa Kifungu cha 25 cha Sheria, Sura 414; nyaraka nyingine zote zilizopokelewa zinapatikana katika ofisi yetu kwa anuani tajwa hapo juu kuanzia saa tatu (3) asubuhi mpaka saa 10:00 jioni. Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa anuani iliyopo hapo juu.

**Limetolewa na:**

**MKURUGENZI MKUU**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI  
(EWURA)**